**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**686** **VITENDO VYA KUJIFUNZA KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka : 2016**

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
3. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

SEHEMU A (Alama 40)

1. Taja aina nne za mazingira ya darasa yanayochangia katika ujifunzaji wa lugha.
2. Fafanua kwa kifupi umuhimu wa mwalimu kuwapa watoto maoni chanya mara kwa mara. (Hoja nne).
3. Eleza kwa kifupi jinsi michezo ya kuigiza inavyosaidia kukuza uwezo wa mtoto wa kuwasiliana. (Mambo manne).
4. Ainisha manufaa manne ya kutumia nyimbo na mashairi katika kufundisha stadi ya kusikiliza.
5. Bainisha matatizo manne ya kimaumbile yanayoweza kuathiri uwezo wa mtoto wa kuzungumza.
6. Kwa nini ni muhimu kwa mwalimu kutumia lugha sanifu na fasaha anapowafundisha watoto? Toa sababu nne.
7. Fafanua kwa kifupi jinsi unavyoweza kutumia matukio ya kila siku darasani (k.m. wakati wa kula) kama fursa za kufundisha lugha. (Hoja nne).
8. (a) Eleza maana ya dhana ya 'upataji lugha'.

   (b) Taja sifa mbili za upataji lugha.
9. Eleza faida nne za kuandaa mapema zana za kufundishia na kujifunzia stadi ya kuandika.
10. Chambua kwa kifupi umuhimu wa mwalimu kuwa msikilizaji mzuri kwa watoto anaowafundisha. (Hoja nne).

SEHEMU B (Alama 30)

11. "Ukosefu wa ushirikiano kati ya wazazi na walimu ni kikwazo kikubwa katika ukuaji wa lugha kwa mtoto." Jadili kauli hii kwa hoja tano.
12. Fafanua kwa kina jinsi utakavyoandaa na kutekeleza shughuli ya "maonyesho na maelezo" ili kukuza uwezo wa watoto wa kuzungumza na kujiamini.
13. "Mazingira ya nyumbani yana mchango mkubwa katika utayari wa kusoma kwa mtoto." Thibitisha kauli hii kwa hoja tano.

SEHEMU C (Alama 30)

14. Eleza hatua tano utakazopitia ili kuongoza darasa la awali katika kuigiza tamthilia fupi kuhusu umuhimu wa usafi.

15. Bainisha faida tano za kutumia vifaa halisi katika kufundisha stadi za lugha na pia taja changamoto mbili.

16. Eleza matayarisho manne ya mwanzo yanayohitajika ili kumfundisha mtoto stadi za awali za kuandika.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***